# Usawiri wa Masuala Mbalimbali ya Kiuhalisia-Hakiki katika Riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* za Euphrase Kezilahabi

*Tusingwire Timon*[1] na *Lenoard Flavian Ilomo*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Kabale*
[2]*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Uhalisia-hakiki ni mtindo wa uandishi ambao mwandishi hushambulia maovu ya jamii bila kuogopa. Katika mtindo huu, mwandishi huchambua maovu yaliyopo kwenye jamii na kuyaweka wazi bila kificho. Hata hivyo, ni waandishi wachache wenye uthubutu huo hasa kama maovu hayo yanawahusu wenye mamlaka moja kwa moja. Makala haya yamechunguza masuala yaliyosawiriwa kiuhalisia hakiki katika riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1974 na 1975 mtawalia. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini teule. Katika kudhihirisha masuala hayo tuliongozwa na Nadharia ya Uhalisia kwa kujikita katika Mkabala wake wa Uhalisia Hakiki. Mkabala huu umejengeka katika wazo kuwa, waandishi wa kiuhalisia hakiki hawaishii tu kusawiri hali kama ilivyo katika jamii, bali huchambua, hukosoa na kusaili hali hizo yameonesha kwamba, masuala ya kiuhalisia hakiki yanayodhihirika kwenye riwaya hizo ni kifo, uwepo wa Mungu, maana ya maisha, uhuru wa mwandamu, na ukahaba.**

**Maneno Muhimu:** *Uhalisia Hakiki, Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Fujo, Kuchambua, Kukosoa*

## Utangulizi

Uhalisia hakiki ni mtindo wa uandishi ambao mwandishi hukashifu maovu ya jamii bila kuogopa (Gorky, 1949). Gorky anaeleza kwamba, katika mtindo wa uhalisia hakiki, mwandishi husawiri jamii iliyo na kusawiri wahusika ambao wnaovuruga utaratibu unaokiuka maadili iyanayotarajiwa katika jamii husika. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba, uhalisia hakiki ni mkabala na mtindo wa utunzi uliotumiwa na wahalisia wakuu wa karne ya 19-20 huko Ulaya na kwingineko kuisawiri jamii. Kadhalika, Mulokozi anaeleza kuwa, watunzi kama Leo Tolstoy (Urusi) na Charles Dickens (Uingereza) walikuwa wahalisia hakiki. Watunzi hao hawakuishia kuonesha tu hali kama ilivyo bali walisaili, walibainisha kukosoa hali hizo katika jamii. Katika Kiswahili, watunzi kama Euphrase Kezilahabi (riwaya za mwanzo) na wengine wengi wa miaka ya 1970-1990 wanaingia katika tapo hili la wahalisia hakiki. Kulingana na maelezo ya Mulokozi, mtindo wa uhalisia hakiki umetumiwa pia na waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Mtindo huu unavyodhihirika katika fasihi ya Kiswahili zaidi ya kudokeza tu. Kutokana na hali hii, watafiti walihamasika kuchunguza udhihirikaji wa uhalisia hakiki ili kufahamu namna mtindo huu unavyojitokeza katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili.

Ili kufanikisha uchunguzi wa udhihirikaji wa uhalisia hakiki katika riwaya ya Kiswahili, tulitumia riwaya teule za Euphrase Kezilahabi. Mwandishi huyu aliteuliwa kwa sababu anatajwa na wataalamu mbalimbali kwamba, ametumia mtindo wa uhalisia hakiki (taz. Mlacha na Madumulla, 1991; Madumulla, 2009; Mulokozi, 2017). Hivyoi, makala haya yamefafanua namna uhalisia hakiki ulivyo katika riwaya teule za Kezilahabi.

### Muhtasari wa Riwaya Teule za Kezilahabi

Riwaya mbili za Kezilahabi ambazo ni *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) zilizotumika katika utafiti uliozaa makala haya. Kwa kuanza na riwaya ya *Kichwamaji*, ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1974. Chapa zingine zilitolewa mwaka 2008 na 2016. Riwaya hii inahusu maisha ya wahusika wawili ambao ni Kazimoto na Manase yanavyoingiliana na watu wengine ambao hawana elimu ya kiwango cha digrii kama walivyo wao. Riwaya hii inachambua suala la maisha kwa ujumla kuhus wahusika hao. Kutokana na mambo mbalimbali yanayowakumba kwenye maisha yao, wanaona kwamba maisha ni kama adhabu na wala hakuna maana yoyote ya kuishi. Mambo ambayo wahusika wa riwaya hii wanakumbana nayo ni pamoja na hofu, magonjwa,

vifo, msongo wa mawazo, kushindwa kupata furaha pamoja na chuki. Mambo haya yanaashiria kwamba katika riwaya ya *Kichwamaji*, mwandishi ameyachambua maisha si tu kuyasawiri kama yalivyo.

Kwa upande mwingine riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1975. Chapa zingine zilitolewa mwaka 2007, 2010, 2013 na 2016. Kwa ujumla, riwaya hii inahusu maisha ya Tumaini na wahusika wengine. Tumaini anaachiwa fedha za kutosha na wazazi wake ambao walijinyima ili wamwachie mali ya kurithi mtoto wao. Tumaini, pamoja na wahusika wengine, wanafanya juhudi mbalimbali za kutafuta furaha. Hata hivyo, wahusika hao hawapati furaha hiyo, na badala yake ndiyo wanazama zaidi katika taabu. Kwa mfano, Tumaini anajaribu kutafuta furaha kwa kuwatumia wanawake kama chombo cha starehe, jambo ambalo linamuingiza kwenye taabu zaidi kama vile kumaliza fedha zake za urithi, kupigwa, na kuhofia kutengwa na jamii. Kutokana na masaibu anayokutana nayo, Tumaini pamoja na Dennis wanahitimisha kwamba dunia ni uwanja wa fujo ambamo kila mtu anazaliwa na kufanya fujo zake, kisha wanapotea (hufa) na kuwaacha wengine nao wafanye fujo zao. Maudhui yanayosawiriwa hapa yanadokeza kwamba katika riwaya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuna masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki.

**Maelezo kuhusu Nadharia Iliyotumika**

Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia kwa kujikita katika Mkabala wa Uhalisia Hakiki. Nadharia ya Uhalisia ilianzishwa katika karne ya kumi na tisa kwa sababu ya kupinga mkondo wa ulimbwende (Uromansia). Kwa mujibu wa Quayson (2000), neno "uhalisia" lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa mwaka wa 1850 ili kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala si kama unavyofikiriwa. Nadharia hii inahusishwa na waasisi mbalimbali. Wamitila (2008) anaeleza kwamba miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Gustave Flaubert (1850) na Erving Goffman (1952). Wamitila anaendelea kueleza kwamba, wataalamu hawa wanashikilia kuwa mtu hufikiria kwa kichwa chake, hafikirii kwa moyo wake. Hii ina maana kuwa, waliwapinga walimbwende katika utungaji wao. Vilevile, wataalamu hawa wanaeleza kuwa Nadharia ya Uhalisia inatumika kwa lengo la kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Wanaendelea kueleza kuwa kazi ya fasihi inapaswa iwakilishe ukweli kwa kutumia maneno halisi, iwe ya kuaminika na iakisi au ioneshe hali halisi katika maisha ya mwanadamu.

Nadharia ya Uhalisia ina mikabala mbalimbali. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mulokozi (2017) mikabala iliyokuwa na nguvu sana katika karne ya 20 ni Uhalisia Hakiki na Uhalisia wa Kijamaa. Hivyo, kulingana na mada ya makala haya tuliongozwa na Mkabala wa Uhalisia Hakiki. Mkabala huu, kwa mujibu wa Mulokozi (keshatajwa), zaidi ya kuwa mkabala, ni mtindo wa utunzi uliotumiwa na wahalisia wakuu wa karne ya 19-20 huko Ulaya na kwingineko kuisawiri jamii. Watunzi kama Charles Dickens kutoka Uingereza na Leo Tolstoy kutoka Urusi walikuwa wana Uhalisia Hakiki kwa sababu hawakuonesha tu hali halisi kama ilivyo bali walisaili, walichambua na kukosoa hali hiyo. Charles Dickens alikuwa mwandishi wa Kiingereza na mwana uhalisia hakiki, yaani mkosoaji wa masuala ya kijamii. Baadhi ya riwaya zake maarufu ni *The Pickwick Papers*, *Oliver Twist*, *Nicholas*, *Nickleby*, *A Christmas Carol*, *David Copperfield*, *Bleak House*, *Little Dorrit*, *A Tale of Two Cities* na *Great Expetations*. Pia, Leo Tolstoy ni Mrusi na mhalisia hakiki anayechukuliwa kama mwandishi bora wa muda wote. Kazi zake maarufu ni: *War and Peace*, *Anna Karenina*, *The Death of Ivan Ilyich*, *The Kingdom of God is Within You* na *Resurrection*.

Aidha, Arabi na wenzake (2022) wanaeleza kwamba, uhalisia hakiki ulikuwa aina mpya ya uhalisia ambapo mwandishi hakuishia tu kuyasawiri maisha kama yalivyo bali alisawiri matatizo ya kijamii kwa kuyakosoa na kuyachambua. Aidha, wanaeleza kuwa uandishi wa aina hii ulijitokeza katika kazi za kifasihi za Maxim Gorky, ambaye alikuwa mwandishi na mwanaharakati wa Kirusi. Gorky alianza kujishughulisha na uandishi kuanzia mwaka 1890 hadi 1936 umauti ulipomfika. Baadhi ya kazi zake maarufu ni *The Lower Depths* (1906) na *Mother* (1906). Kwa ujumla, kulingana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, barani Ulaya uhalisia hakiki ulianza karne ya 18 na kuendelea. Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, Madumulla (2009) anaeleza kwamba, uhalisia hakiki ulianza kujitokeza miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 ambapo ndoto na matarajio kuhusu kuifikia nchi ya ahadi ya Azimio vilianza kufutika. Hali ya uchumi ya wananchi ilianza kudidimia.

Idadi kubwa ya vijiji vya ujamaa na makazi mapya yaliyokuwa yameanzishwa yalianza kusuasua katika miaka ya 1970. Madumulla anasema, hali hii ndiyo ilisababisha kuibuka kwa nathari bunilizi ambazo zilielekeza kidole cha mashtaka kwa viongozi wa serikali kwa uroho wao, usaliti na rushwa. Viongozi hawakutaka kuwasaidia viongozi wadogo ambao walikuwa na imani katika ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Mifano mizuri ya riwaya zilizotumia mtindo huu ni riwaya ya *Nyota ya Huzuni* (1978) na *Njozi Iliyopotea* (1979). Madumulla anasema, zipo riwaya zingine ambazo zilisaili hali ya maisha ilivyokuwa ikiendelea. Mifano ya riwaya hizo ni *Kichwamaji* (1974) na *Gamba la Nyoka* (1979) za Kezilahabi. Maelezo haya yanaonesha kwamba, riwaya zilizotungwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 hazikuishia tu kusawiri masuala ya kisiasa na kijamii bali pia zilikosoa.

Msingi mkuu wa Mkabala wa Uhalisia Hakiki ni kuchambua, kusaili na kukosoa hali iliyopo katika jamii. Hivyo, ili kuchambua data za makala haya, tumejiegemeza katika msingi huo.

**Masuala ya Kiuhalisia Hakiki katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi**

Katika makala haya masuala ya kiuhalisia hakiki yanayodhihirika ni yale mambo ambayo mwandishi hajaishia tu kuyasawiri kama yalivyo katika jamii bali ameyachambua, ameyakosoa na kuyasaili katika riwaya teule. Kwa ufupi, utafiti uliofanyika umegundua kuwa riwaya teule za Euphrase Kezilahabi zimetumia mtindo wa uhalisia hakikiili kujadili masuala anuwai ya kijamii hususan suala la kifo, uwepo wa Mungu, maana ya maisha, uhuru wa mwanadamu na ukahaba. Sehemu hii imechambua masuala hayo moja baada ya jingine kama ifuatavyo:

**Suala la Kifo**

Kifo ni tukio ambalo huwakumba wanajamii kila uhao na halikwepeki. Ingawa kifo kimekuwapo tangu kuumbwa kwa binadamu na hakiepukiki, bado kimeendelea kuwaogofya wale wanaobaki. Sababu ni kwamba, wale wanaokufa huwa hawarudi wala hawajawahi kurudi ili kueleza kuhusu kifo. Kwa hiyo, mambo yanayohusu kifo yamebakia kuwa na mijadala isiyoisha. Baadhi ya mijadala hiyo ni kuwapo kwa maisha baada ya kifo, kuwapo kwa hukumu baada ya kifo, mahali roho inapokwenda baada ya mtu kufa na namna mtu anavyokifikia kifo. Utafiti huu umebaini kuwa kifo ni miongoni mwa masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya teule za Kezilahabi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), Kezilahabi anasaili mawazo yaliyopo kuhusu kifo kwamba hutokea mara moja. Kezilahabi anasaili mawazo hayo na kuonesha kuwa hayana ukweli. Kwa mtazamo wake, mwanadamu huanza kufa mara tu anapozaliwa ingawa anaweza kujiona yupo sawa. Kezilahabi anatueleza haya katika dondoo lifuatalo:

> Ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa pole pole. Watu wengi wanafikiri kwamba sisi wanadamu tunakufa mara moja. Hili ni jambo la uongo. Tangu mwanadamu anapozaliwa anaanza kufa pole pole ingawa yeye mwenyewe anajiona yu sawa. Siku zake zinakatwa moja moja. Kaburi ni hatua yetu ya mwisho tu. Kazimoto, tunapoishi tunakufa pole pole, kwahiyo kufa ni kuishi.
>
> Sikuweza kufuata vizuri ufafanuzi wako. Lakini nafikiri katika maneno yako ya mwisho umenivungavunga mahali fulani.
>
> Unafikiri unaishi? aliniuliza.
>
> Ndiyo, nilimjibu.
>
> Unafikiri kwamba humo katika hali ya kufa?
>
> Hapana
>
> Unafikiri wewe ndiye Kazimoto niliyemwona miaka kadhaa iliyopita? Labda hujitambui. Nakuona umekonda sana siku hizi.
>
> Nakubali kwamba nimebadilika.
>
> Mabadiliko hayo ndiyo yanakufanya uwe unakufa pole pole. Kaburi ni hatua ya mwisho tu ya tendo lile lile.
>
> Utaniambia nini juu ya wale wanaokufa wangali bado watoto wadogo?

> Wakiwa katika hali hii ya kufa pole pole huwa kitu fulani ndani hakiendi sawa. Kwa hiyo hatua yao ya mwisho inafika kabla ya wakati. Kama uonavyo watu wengine wanapata ndevu wangali na umri wa miaka saba.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 186).

Katika dondoo hili, Kezilahabi anakosoa mawazo ya watu wengi kuhusiana na namna mwanadamu anavyokufa. Watu wengi hufikiri kuwa mwanadamu anakufa mara moja, yaani kwamba kifo ni kama ajali. Kwa upande wake anasema, hili ni jambo lisilo sahihi kwa sababu mtu hakifikii kifo kama ajali, bali hukifikia kifo polepole kutokana na siku zake kuwa zinakatwa polepole kiasi cha yeye mwenyewe kutotambua. Aidha, Kezilahabi anabainisha sababu za watu wengine kufa mapema kwamba katika hali ya kufa polepole kuna kitu fulani kinaweza kuingilia na kusababisha siku za mtu zikakatwa haraka haraka.

Kwa mfano, Rukia anakufa mapema kuliko, mama yake, baba yake (Mafuru), mdogo wake (Kalia) na kaka yake (Kazimoto) kwa sababu ya kukataa kula baada ya kutiwa mimba na Manase. Dondoo lifuatalo linathibitisha maelezo haya:

> Kazimoto, Tuza alisema, ndugu yako amekufa kwa sababu amekosa nguvu; alikuwa hajala vizuri kwa muda mrefu uliopita.
>
> Hayo usemayo ni kweli, nilimwambia
>
> Amekufa akitaja jina lako.
>
> Alisema nini kuhusu jina langu?
>
> Alikulilia; akikuomba umsamehe kwa yale yote yaliyotokea kwake.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 83).

Dondoo hili linaonesha kwamba, Rukia alikufa kwa sababu ya kitendo chake cha kutokula. Kulingana na Kezilahabi, siku za Rukia za kuishi zilianza kukatwa haraka tofauti na watu wengine katika familia yake kutokana na kitendo hicho. Hivyo, kutokula ni miongoni mwa mambo yanayoweza kumsababishia mtu siku zake za kuishi kukatwa kwa kasi.

Vilevile, kitendo cha Kazimoto kuendekeza ngono kwa kutembea na wanawake ambao ni wahudumu wa baa kinamsababishia ugonjwa. Matokeo ya ugonjwa huo ni pamoja na kuzaa mtoto mwenye kichwa kikubwa kuliko kawaida. Kitendo hiki kinamfanya Kazimoto ajiue mwenyewe. Hivyo, anakufa mapema kuliko Sabina, mkewe ambaye amemzidi mwaka mmoja, pamoja na baba yake (Mafuru). Kazimoto aliacha ujumbe ufuatao kabla ya kujiua:

> Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili ni nini? Pia nikiwa duniani sikupata kukutana hata siku moja na mtu anayeamini kwamba kuna Mungu. Watu wanaoogopa kufa na kwenda motoni hao nimewaona, tena wengi sana. Mtu yeyote asilaumiwe kwa kifo changu. Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 195).

Dondoo hili linaonesha kwamba, Kazimoto kwa mawazo yake na matendo yake katika kuishi kwake ameyafanya maisha kuwa mafupi kwa kukata siku zake haraka, yaani matendo yake yamemfanya kufa kabla ya watu wanaomzidi kwa umri kama Mafuru, Kabenga, Tuza, Tegemea na Sabina.

Kupitia vifo vinavyotokea katika familia ya Mafuru, Kezilahabi anaonesha kwamba kifo hakitokei mara moja, yaani kama ajali bali mtu kwa matendo yake huzifanya siku zake za kuishi ziwe finyu kuliko hata ambao ni wakubwa kwake kiumri. Hii imejidhihirisha kupitia namna vifo vya wanafamilia wa Mafuru vilivyotokea ambao ni Rukia, mama Kazimoto (mke wa Mafuru), Kalia na Kazimoto. Kila mtu kifo kimempata kulingana na matendo yake ambayo yamesababisha kukata siku zake haraka kuliko kawaida. Sambamba na hayo, matendo yote mabaya yanaweza kuwa sababu ya kupunguza siku za kuishi lakini kuna yale ambayo yanapunguza kwa kasi na yale ambayo yanapunguza kwa kasi zaidi. Kwa mfano, matendo ya Kalia ya kubaka yanapunguza kwa kasi zaidi

siku za kuishi kutokana na mwitiko wa jamii dhidi ya matendo hayo, na ndiyo maana Kalia anauawa na watu kutokana na tabia hiyo. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba wakati Kalia anaanza kubaka wanawake, Kazimoto alikwishaanza kutembea na malaya kama vile Nyabuso kwa muda mrefu. Pamoja na matukio yake hayo ya kutembea na malaya, siku zake hazikupungua kwa kasi hadi pale alipoambukizwa ugonjwa na Pili mfanyakazi wa baa, ugonjwa unaoanza kuonesha madhara baada ya miaka kumi na minne hivi au zaidi. Manase anamweleza haya Kazimoto akisema:

> Manase alinieleza kwamba ugonjwa huo ulikuwa hauwezi kutambulika kwa urahisi. Alisema kwamba ugonjwa huo unaingia ndani ya damu na kukaa bila kumdhuru mhusika. Baada ya miaka kumi na minne hivi au zaidi unaanza kumdhuru mhusika, lakini kabla yake ni vigumu kuusikia. Alinieleza jinsi daktari mmoja alivyogundua ndani ya damu yake na kueleza jinsi unavyoweza kuharibu kizazi kimoja hadi kingine.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 192).

Dondoo hili linaonesha kwamba, licha ya mtu kupata ugonjwa ana uwezo wa kuishi nao kwa miaka kumi na minne au zaidi. Hii ina maana kwamba, hata Kazimoto kama asingejiua bado alikuwa na miaka kadhaa ya kuishi kwa sababu bado dalili za ugonjwa huo zilikuwa hazijaanza kuonekana kwenye miili yao zaidi ya kuzaa mtoto mwenye kichwa kikubwa. Kimsingi, ukilinganisha mtu ambaye amepata ugonjwa huu na mtu ambaye anabaka wasichana mara kwa mara. Bila shaka yule anayebaka ni rahisi kuuawa na wananchi wenye hasira kali ilhali yule ambaye amepata ugonjwa bado anasubiri miaka kumi na minne au zaidi ndiyo siku zake zianze kukatwa kwa kasi.

Kuhusu suala la kifo katika riwaya ya *Kichwamaji*, Kezilahabi anakosoa watu wanaodhani kwamba kifo hutokea kama ajali. Kwa upande wake anaona kwamba mtu hufa polepole bila yeye mwenyewe kujijua. Hata hivyo, anatahadharisha kwamba mtu mwenyewe anaweza kuzifanya siku zake badala ya kukatwa polepole zikawa zinakatwa harakaharaka kama tulivyoona matendo ya Rukia, Kalia na Kazimoto yanavyosababisha siku zao kukatwa haraka kuliko Mafuru aliyewazidi umri. Ukosoaji huo kuhusu namna kifo kinavyotokea unaakisi mawazo ya Mkabala wa Uhalisia Hakiki kwamba, mwandishi wa kiuhalisia hakiki haishii tu kusawiri hali ilivyo, bali pia huchambua na kukosoa

Aidha, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), bado Kezilahabi anaendeleza wazo kwamba mwanadamu hufa polepole bila yeye mwenyewe kutambua. Katika riwaya hii anaenda mbele zaidi kwa kusema kwamba miaka ni kama kunguni anavyomnyonya mtu taratibu na kumwacha ajifie mwenyewe. Kezilahabi anathibitisha wazo hili anaposema:

> Mungere hakunung'unika: alifahamu kwamba mumewe hakuwa mvivu. Alifahamu kwamba miaka ni kama kunguni; inamnyonya mtu pole pole, halafu huacha gofu kuanguka kaburini.
>
> **Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975:6).

Dondoo hili linaonesha kwamba kadiri miaka inavyozidi kusonga mbele ndivyo afya ya mtu inavyoendelea kuzorota. Baada ya hapo humwacha mtu huyo, na kwa kuwa afya yake imedorora vya kutosha kulingana na miaka yake mtu huyo hufa mwenyewe. Utafiti huu unakubaliana na Kezilahabi kwamba kadiri miaka ya mtu inavyozidi kuongezeka ndivyo afya yake inavyozidi kuwa mbaya. Hii inajidhihirisha kupitia wazee mbalimbali hasa wenye miaka themanini na kuendelea. Kwa mfano, ukitazama ngozi zao tu utaona kwamba zimekunjamana na wengine hawawezi kutembea bila fimbo. Yote haya yanaonesha kwamba miaka imenyonya afya zao na si muda mrefu watajifia wenyewe na kutumbukizwa kaburini kama Kezilahabi anavyosema.

Matokeo ya utafiti huu yanaakisi msingi wa Mkabala wa Uhalisia Hakiki kwamba, mwandishi wa kiuhalisia hakiki haishii tu kusawiri hali ilivyo, bali pia huchambua na kukosoa hali hiyo. Haya ndiyo tunayoyaona katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Kezilahabi haishii tu kusawiri vifo vya wahusika kama Kapinga na Munyago, bali anachambua na kuona kwamba kadiri mtu anavyozidi kuishi ndivyo anavyokikaribia kifo au kulisogelea kaburi.

Pia, Kezilahabi anasaili imani mbalimbali zilizopo miongoni mwa watu zinazoeleza kwamba wanaotenda mema hapa duniani watalipwa mema ilhali wale wanaotenda mabaya watapata adhabu

baada ya kifo. Kwa mujibu wa Mbiti (1969), katika dini ya, waumini wa dini hiyo wanaamini katika ufufuo baada ya kifo ambapo watenda mema wataenda mbinguni na kuishi na Mungu huku waasi wakitupwa katika moto wa milele. Vilevile, dini ya Kihindi inashikilia kuwa kuna kuzaliwa upya kwa kiumbe baada ya kifo kutegemeana na matendo yake katika maisha ya awali, yaani kabla ya kifo (Sivananda, 1997). Sivananda aneleza kwamba, mtu aliyeishi maisha mema huzaliwa katika tabaka la juu ilhali aliyeishi maisha ya uovu huzaliwa katika tabaka la chini. Kadhalika Odongo (2014) anaeleza kuwa, dini ya Kiislamu inashikilia kuwa kuna adhabu baada ya kifo kwa wale wanaotenda mabaya huku wema wakizawadiwa. Kezilahabi anakosoa imani hizi ambapo anajikita zaidi kwenye kukosoa imani ya dini ya Kikristo ambayo waumini wake wanaamini kuwa wema huenda mbinguni, ambapo anasema kwa sasa ana mawazo tofauti na hayo. Mwandishi anayasema haya kama inavyooneshwa katika dondoo lifuatalo:

> Zamani, Dennis alisema, hata mimi nilifikiri kwamba maisha mazuri sana, na kwamba watu wema huenda mbinguni; lakini sasa nina mawazo tofauti kabisa na yale ya zamani. Ulimwengu siku hizi ninauona kama meza-kama meza hii ya kulia unayoiona sasa. Sisi wanadamu tu kama majani. Tunaanguka kutoka juu mtini; tunakuja tunapepea angani kama unyoya namna hii na kuanguka juu ya meza ta! Hakuna atakayerudi juu mtini.

**Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975: 64)**.**

Dondoo hili linaonesha namna mwandishi anasaili imani kwamba, kuna maisha baada ya kifo na kwamba kuna kitu kinaitwa mbingu kwa wale wanaotenda mema. Kwa upande wake anaona kwamba, baada ya kifo, habari za mwanadamu zinaishia hapo hapo, hakuna uhai tena. Anaeleza haya kwa kufananisha na namna jani linavyoanguka kwenye mti, hakuna siku litapata tena uhai au kurudi katika mti. Usaili wa namna hii unaakisi Mkabala wa Uhalisia Hakiki unaosema kwamba mwandishi wa kihalisia hakiki haishii tu kusawiri hali ilivyo bali pia huikosoa na kuisaili. Kwa mfano, watu wanaotenda mambo mema kwa matarajio ya kuwapo kwa mbingu watakakopewa mataji ya matendo yao mema, mwandishi anasaili matarajio hayo kwa kumtumia mhusika, Dennis. Kulingana na maelezo yake mtu akifa amekufa na wala hakuna mbingu kwa watenda mema wala adhabu kwa watenda maovu. Kwa ujumla, ukosoaji huu unakatisha tamaa watu wanaotenda mema na wakati mwingine kuchochea maovu kwa sababu watenda mema wataona hakuna faida yoyote ya kufanya hivyo. Suala hili la wahalisia hakiki kukatisha tamaa linazungumziwa pia na Mulokozi (2017). Mulokozi anaeleza kwamba waandishi wa kihalisia hakiki kama Charles Dickens na Leo Tolstoy walikosoa hali mbalimbali katika jamii zao na wakati mwingine walikosoa hali hizo kwa hali ya kukatisha tamaa.

**Suala la Uwepo wa Mungu**

Wabantu ni watu wanaoamini uwepo wa Mungu (Mbiti, 1969). Maelezo ya mtalaamu huyu yamethibitishwa na wataalamu mbalimbali waliofanya tafiti zao katika jamii za Kibantu. Miongoni mwao ni Raphael (2018) katika ngano za jamii ya Waha, Duwe (2020) katika mbolezi za Wangoni, Sanga (2020) katika mbolezi za Wakinga, na Ally (2022) katika ngano za Wadigo. Kezilahabi katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), anawatumia wahusika kusaili imani ya Wabantu wenzake wanaoamini kwamba kuna Mungu. Uwepo wa Mungu ni miongoni mwa masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya teule za Kezilahabi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* Kezilahabi anakosoa watu wanaoamini kwamba kuna Mungu ambapo anasema wamejiamulia wenyewe katika milango yao ya fahamu. Mwandishi anatuibulia wazo hilo kupitia mhusika Kazimoto anapomwambia Manase maneno haya:

> Unaona, Manase; mwanadamu ameamua kwamba kuna Mungu kwa sababu ya hali yake ya woga iletwayo na milango ya fahamu. Kwa hiyo mtu anayeamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuaye kwa kufuata milango ya fahamu zake.

**Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 124).

Katika dondoo hili, mwandishi anakosoa wale ambao wanaamini kwamba Mungu yupo. Kwa upande wake anachambua suala hili na kuona kuwa mwanadamu amejiamulia mwenyewe kwamba

kuna Mungu kwa sababu ya woga wake uletwao na milango ya fahamu. Hii inaashiria kwamba mwandishi haishii tu kusawiri imani iliyopo katika jamii juu ya Mungu, bali anaichambua na kubaini kwamba kuibuka kwake kumetokana na woga wa mwanadamu mwenyewe. Pia, kutokana na masaibu anayokutana nayo Kazimoto, ikiwamo kufiwa na mtoto wake ambaye aliishi saa moja tu baada ya kuzaliwa, mhusika huyu anaanza kutilia shaka kama Mungu kweli yupo. Rejea dondoo lifuatalo:

> Usiku nikiwa na mke wangu, mawazo mengi yalinijia kichwani. Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli Mungu alikuwapo sikuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Matumaini yetu yote; kazi na taabu tuliyopata-yote hayo chini! Sikuona maana ya maisha.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 180).

Katika dondoo hili, Kazimoto anaeleza namna alivyopokea kifo cha mtoto wake aliyekaa saa moja tu baada ya kuzaliwa. Hapa ndipo Kazimoto alipoanza kujiuliza na kufikiria kama kweli Mungu yupo. Kulingana na mawazo haya ina maana kuwa, kama Mungu angekuwepo asingeruhusu kifo cha mtoto wake ambaye walikuwa wanamsubiri kwa hamu kubwa. Uchambuzi wa suala la imani kuhusu uwepo wa Mungu unathibisha kwamba hili ni miongoni mwa masuala yaliyohakikiwa kwa sababu mwandishi anakosoa imani ambazo zimekuwapo miaka na mikaka, imani ambazo zimeendelea kushikiliwa na kurithishwa kwa vizazi na vizazi.

Makala haya yanakubaliana na Kezilahabi kuhusu mtazamo wa baadhi ya watu kwamba huenda hakuna Mungu. Hii ni kwa sababu ya masaibu ambayo wanadamu wanapitia chini ya jua. Kwa mfano, watu mbalimbali makanisani na misikitini wameomba Mungu anusuru suala la vita vya Urusi na Ukreni, lakini bado hadi sasa vinaendelea. Pia, watu mbalimbali wameomba Mungu ainusuru Uturuki dhidi ya matetemeko makubwa ya ardhi lakini bado yanaendelea kuwa tishio. Masuala haya yanatosha kwa mwanadamu kutilia shaka uwepo wa Mungu.

Pia, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Kezilahabi anasaili imani zinazomtambua Mungu kama amejawa na rehema, huruma na upole. Anakosoa mtazamo kuwa Mungu ni mwenye huruma kwa kuonesha kwamba, kwa vyovyote hana huruma kwani anamwacha mwanadamu anateseka hapa duniani. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Tumaini anamweleza John na Anastasia namna anavyoteseka na maumivu na hajui amemkosea nini Mungu. Dondoo lifuatalo linathibitisha maelezo haya:

> "John," Tumaini aliita. "Anastasia! Mimi si mtu tena kama ninyi. John mimi sasa ninakufa. Niacheni nife peke yangu. Anastasia! John! Sijui nifanye nini. Sijui nimemkosea nini Mungu!" Tumaini alitikisa kichwa chake kwa maumivu.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 97)

Dondoo hili linabainisha kwamba, Mungu anampa mateso Tumaini ilhali mwenyewe hajui amemkosea nini. Katika hali kama hii majina yanayomrejelea Mungu kama mwenye rehema, mpole na mwenye huruma yanakosolewa kwa kuwa hayana uhalisia kwa sababu hamuonei huruma Tumaini kwa maumivu anayoyapata. Kwa mantiki hii, mwandishi anakosoa majina mazuri anayopatiwa Mungu kwamba inaelekea anapewa bila ya jasho, yaani hakuna kazi dhahiri zinazohalalisha majina hayo. Kwa mfano, kama Mungu ni mwenye rehema, mpole na mwenye huruma kwa nini asimhurumie na kumuondolea Tumaini mateso?

Suala la Mungu kurejelewa kama mwenye huruma linazua mashaka hasa pale unapowaona watu wakipitia matatizo mbalimbali. Ikiwa tunaendelea kushikilia imani kwamba Mungu ni mwenye rehema, mpole na mwenye huruma, basi ni kwa baadhi ya watu wala si wote, au Mungu alikuwa hivyo zamani wakati zilipoasisiwa dini zinazomrejelea Mungu kwa majina hayo, ikiwemo dini za Kikristo na Kiislamu.

**Suala la Maana ya Maisha**

Maisha ni muda ambao kiumbe hai anajaliwa kuishi. Utafiti huu ulibaini kwamba maana ya maisha ni miongoni mwa masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya teule za Kezilahabi. Hii ni kwa sababu Kezilahabi haishii tu kusawiri kipindi ambacho mwanadamu anaishi, bali anakichambua

kipindi hicho cha kuishi kwake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), Kezilahabi anachambua maisha na kuyaona kama adhabu ambayo Mungu amempatia mwanadamu. Kupitia mhusika Kazimoto, Kezilahabi anatuthibitishia mtazamo wake anaposema:

> Maisha ambayo hayashibwi wala kuridhishwa. Zaidi ya hayo mwenye nguvu anatunyang'anya maisha haya wakati wowote bila hata kutuarifu. Kweli, mfano wa adhabu hii kali ni yule mtu aliyeamrishwa kujaza maji ndani ya pakacha. Na sisi wanadamu tumekubali kufanya hivi kwa jina la 'Furaha'. Maisha matamu! Yaani adhabu ni tamu. Ndiyo kusema tuna akili kweli wanadamu? Maswali haya yalinizunguka sana kichwani. Mara fulani niliamua kwamba mwanadamu hana akili. Kama angekuwa na akili angekataa adhabu hii
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 84).

Dondoo hili linaonesha mwandishi, kupitia mhusika Kazimoto, anawakosoa vikali watu wanaosema maisha ni matamu ilhali ni adhabu. Anayafananisha maisha na mtu ambaye amepewa adhabu ya kujaza maji kwenye pakacha, kwamba licha ya mwanadamu kujaribu kwa kila njia kutunza uhai wake lakini hajawahi kufanikiwa. Kwa sababu hiyo, mtu hawezi kukiepuka kifo kinapomjia. Kwa hiyo, Mungu amempa mwanadamu adhabu ya kutunza maisha yake ilhali hawezi hata kuyatunza. Adhabu hii ni kali kwani kifo na uhai huwa haviachani. Muda wote ambao mwanadamu anakuwa hai, basi hutembea na kifo. Ni kwa msingi huu, mwandishi anashangaa mwanadamu anavyofurahia adhabu hiyo ya kutunza maisha kwa madai kwamba ni matamu. Aidha, maelezo ya mwandishi kupitia mhusika Kazimoto, yanabainisha kwamba maisha si matamu kama watu wengine wanavyoyachukulia. Utafiti huu unakubaliana na mwandishi kwamba maisha ni adhabu, na adhabu yenyewe ni kuyatunza. Hii ni kwa sababu mwanadamu muda wote anafanya juhudi ya kuhakikisha kwamba anakuwa hai lakini cha kusikitisha ni kwamba anao uwezo mdogo sana wa kuyatunza.

Aidha, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Kezilahabi anachambua maisha na kubaini kwamba maisha ni fujo za kuchezeka jukwaani. Baada ya kufanya fujo hizi, binadamu huondoka jukwaani (yaani huaga duniani); hivyo, mchezo huu wa kuigiza uliokuwa unaendelea hufikia mwisho. Kezilahabi anatuibulia suala hili kupitia mhusika Dennis ambaye anasema:

> Zamani, niliamini kwamba kila mwanadamu ameumbwa kuja hapa duniani ili apate kufurahia ulimwengu kiasi awezavyo kabla hajafa. Lakini sasa ninaamini kwamba **Dunia Uwanja wa Fujo**. Kila mwanadamu ameumbwa kuja kufanya fujo yake halafu anajiondokea na kupotea. Kuna fujo za aina nyingi. Watu wengine wamefanya fujo zaidi ya wengine.
>
> **Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975: 63).

Nukuu hii inaonesha kwamba mwandishi amebadili mtazamo wake kuhusu maisha ambapo awali alidhani kwamba maisha ni furaha lakini, kwa sasa anaamini kwamba maisha ni fujo. Hii inamaanisha kuwa mtu huumbwa ili aje afanye fujo zake halafu muda wake ukiisha anakufa. Katika fujo hizi kuna wale wanaofanya fujo zao zikajulikana na wengine hazijulikani kabisa.

**Suala la Uhuru wa Mwanadamu**

Uhuru ni hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine; hali ya kufanya mambo bila kuingiliwa (TUKI, 2019). Uhuru unaweza kumhusu mtu binafsi au nchi nzima. Aidha, uhuru humwezesha mtu kujitawala kiakili, kidini na kimaadili. Kisiasa karibu nchi zote zipo huru. Kwa upande wa kidini, Wakristo wanaamini kwamba wapo huru baada ya Yesu kuja kuwakomboa. Kwa mantiki hiyo, wanaamini kwamba si watumwa tena wa shetani. Utafiti huu umebaini kwamba uhuru wa mwanadamu ni miongoni mwa masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya teule za Kezilahabi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), Kezilahabi anachambua suala la uhuru na kuona kwamba mwanadamu hawezi kuwa huru kwa sababu suala la upendo limeondoa uhuru wa mwanadamu. Mathalani, Kazimoto anakosa uhuru wa kufurahi na wasichana kwa sababu anapaswa kupenda familia yake kuliko wasichana. Mazungumzo baina ya Mafuru (baba yake Kazimoto) na Kazimoto yanathibitisha hoja hii:

> "Kazimoto, mambo ya wasichana yamekuingilia vile kwamba watu wa nyumbani umewasahau."
> "Mambo ya wasichana sihusiani nayo"
> "Unasema nini? Mtoto gani wewe? Unataka kunidanganya mimi? Kazimoto uongo huu wote ulipata wapi? Unafikiri mimi sikukuona unanyatia mihogoni?"
> "Basi, basi baba, nisamehe," nilisema upesi.
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 36)

Dondoo hili linaonesha kuwa, Kazimoto anaingiliwa kwenye starehe ya kupenda wasichana kwa sababu ya jukumu la kuipenda familia yake na kuitunza. Masuala ya kifamilia ni chanzo kikubwa cha watu kutokuwa huru.

Zaidi ya hayo, Kezilahabi anachambua suala la uhuru na kubaini kuwa upendo wa wazazi kwa watoto ni chanzo kimojawapo cha kukosekana kwa uhuru. Mathalani, mazungumzo baina ya mama Kazimoto na Kazimoto mwenyewe yanadhihirisha kwamba Kazimoto hana uhuru wa kufanya chochote kwa sababu ya upendo wa mama yake. Rejea mazungumzo yao katika dondoo lifuatalo:

> Mama aliingia mkono nyuma kama mtu aendaye kilioni. "Ulikuwa wapi?" aliuliza kwa upole
>
> Mimi nilinyamaza kwa sababu mara nyingi nilikuwa nimemwambia asiniulize swali kama hilo.
>
> "Kazimoto ulikuwa wapi kwa muda wa siku mbili zilizopita? Uliondoka bila kutuarifu na kurudi kwenyewe unarudi usiku wa manane. Umezaliwa, Kazimoto na kuna watu wanaokujali"
>
> "Unataka nini" nilimwambia.
>
> "Kazimoto, fahamu kwamba mimi ninakupenda sana, huwezi kuondoka bila kunipasha habari. Ungeuawa je- tungemshuku nani?"
>
> "Mapenzi ya kitoto namna hiyo mimi siyapendi. Kila siku niondokapo nyumbani unaniuliza "unakwenda wapi?" Mimi nimekwisha kuwa mtu mzima sasa, na sitaki wewe uwe unafahamu njia zangu zote. Hata kama nikiwa nakwenda kwa wanawake unataka nikueleze?"
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 64)

Dondoo hili linaonesha wazi kwamba, Kazimoto anatamani kuwa huru lakini hawezi kuupata uhuru huo kwa sababu ya upendo wa mzazi wake. Upendo huo unamtaka Kazimoto amjuze mzazi wake kila anachokifanya. Kitendo hicho hakimpendezi Kazimoto kwani anaona kwamba anachungwa kiasi cha kushindwa kufanya mambo ayatakayo. Hali hii inaonesha wazi kwamba Kezilahabi anakosoa upendo wa wazazi uliopitiliza kwani huwafanya watoto wao kukosa uhuru.

Aidha, Kezilahabi anachambua suala la uhuru wa mwanadamu na kuona kuwa hakuna mwanadamu ambaye yupo huru na maisha yake kwa sababu Mungu anaweza kukunyang'anya maisha hayo bila hata kutoa taarifa. Mwandishi, katika riwaya ya *Kichwamaji*, anatumia uzungumzinafsiya wa Kazimoto kuhusu maisha ambapo anasema: "Zaidi ya hayo mwenye nguvu hutunyang'anya maisha haya wakati wowote bila hata kutuarifu" (uk. 84). Kezilahabi anaonesha hali ya uhuru wa maisha kwa namna ya kukatisha tamaa kwa sababu hata kama mtu ana malengo yake katika maisha, Mungu huingilia uhuru huo kwa kumnyang'anya mtu huyo maisha yake. Kadiri mwanadamu anavyofikiria kuhusu namna atakavyonyang'anywa uhai, ndivyo uhuru unavyopotea zaidi, kwani hufikiri atanyang'anywa lini, wapi, na kwa sababu gani bila kupata majawabu.

Pia, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Kezilahabi anachambua suala la uhuru wa mwanadamu na kutueleza kwamba zamani alifikiri mwanadamu ndiye kiumbe pekee mwenye furaha na uhuru. Hata hivyo, kwa sasa (wakati anaandika riwaya hii) alikuwa na mtazamo tofauti na ule wa zamani kuhusu suala la uhuru wa mwanadamu. Rejea dondoo lifuatalo kwa ufafanuzi zaidi:

> Zamani, nilifikiri kwamba mwanadamu ndiye kiumbe pekee mwenye furaha na uhuru. Sasa nimeona kwamba kati ya viumbe mwanadamu

> ni wa mwisho katika mambo haya mawili. Nyumba kubwa hii uionayo haiwezi kuniletea furaha Tumaini. Kusema haki, hii hali ya kila kiumbe kutafuta mahali pa kulala yadhihirisha wazi kwamba viumbe hawapendi uhuru. Tunapenda kujifungia wenyewe kwa kusema kwamba eti tunatafuta malazi au kujikinga. Kadri nionavyo mimi nyumba za binadamu zaonyesha upungufu wa uhuru alionao; na kadiri tujengavyo nyumba nzuri zaidi ndivyo tujifungiavyo zaidi jelani.
>
> **Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975: 64)

Maelezo ya Dennis katika dondoo hili, yanaonesha namna Kezilahabi anavyochambua suala la uhuru. Kezilahabi anaona kwamba kitendo cha kujenga nyumba hasa nyumba nzuri ni ishara kwamba binadamu hawapendi uhuru. Hata hivyo, anamkosoa mwanadamu kwa kujifungia katika eneo moja kwa mwamvuli kwamba anatafuta malazi. Hali hii inadhihirisha alichokisema Badru (2019) kuwa kufikia uhuru kamili ni njozi kwa sababu binadamu 'hata akifanikiwa kupigana na nguvu zilizo nje yake na kushinda, bado atajifunga yeye mwenyewe' (uk. 505). Kwa mfano, ukilinganisha uhuru wa mpangaji wa nyumba na mwenye nyumba, unaweza kuona kwamba angalau mpangaji yeye ana uhuru kidogo kuliko mwenye nyumba. Hii ni kwa sababu kwa upande wa mpangaji, walau anaweza kuhama muda wowote ilimradi tu ana pesa lakini mwenye nyumba si rahisi kuhama muda wowote kwa sababu hapo ndipo anapopachukulia kama malazi yake ya kudumu. Kwa hiyo, kulingana na mwandishi, tunaweza kusema mtu ambaye yupo huru ni kichaa ambaye hana nyumba wala makazi; kwa hiyo, anaweza kulala mahali popote.

Sambamba na hayo, Kezilahabi anaona kwamba zoezi endelevu la kumwabudu Mungu limesababisha kupotea kwa uhuru. Kutokana na kumhofia Mungu, mwanadamu hawezi kufanya chochote anachojisikia kwa madai kwamba Mungu hapendi. Kwa mfano, Tumaini katika ujumbe alioandika gazetini, anaeleza namna wakuu wa dini walivyopinga watu kwenda ufukweni kuonyeshana uchi wao licha ya serikali kutosema neno lolote. Tumaini anatueleza kwamba:

> ...vyama mbalimbali vimekwishaanzishwa katika nchi hizi. Wanachama huenda ufukweni, huonyeshana uchi wao kwa raha bila serikali kusema neno lolote. Wakuu wa dini walivipinga vyama hivi; lakini miongoni mwa wanachama kulikuwa ni walimu wa vyuo vikuu- hawa walimu waliwajibu wakuu wa dini kwa kusema: Sisi tunafuata uhuru kamili wa binadamu, mwanadamu hawezi kujidai kwamba yeye ni huru kama bado anatawaliwa na hofu ya uchi wake...
>
> **Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975: 74)

Dondoo hili linaonesha kwamba watu walikuwa wanaenda ufukweni kuoneshana uchi kwa raha bila kikwazo chochote kutoka serikalini lakini wakatokea wakuu wa dini ambao walipinga tabia hiyo. Bila shaka, upingaji huo ulitokana na hofu kwamba walikuwa wanatenda dhambi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa mwandishi, bila dini pengine watu wangekuwa na uhuru kwa kutokuwa na hofu yoyote ya kumkosea Mungu. Hii ina maana kwamba mwanadamu anaweza kupata uhuru endapo ataondoa wazo la kuwapo kwa Mungu na nguvu zake ambazo ndizo zinamwekea mwanadamu mipaka katika suala la uhuru. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba suala la uhuru wa mwanadamu ni miongoni mwa masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki kwa sababu mwandishi hajaishia tu kusawiri uhuru kama unavyojitokeza katika jamii, bali anachambua na kukosoa mambo mbalimbali yanayohusiana na uhuru na kuweka bayana vikwazo vya mwanadamu katika harakati za kutafuta uhuru.

**Suala la Ukahaba**

Khalid (1982) anaelezea kuhusu kahaba kuwa ni hali ya mwanamke au mwanamume kushiriki mapenzi na watu tofautitofauti kwa matarajio ya kupata fedha au zawadi bila kuwa na hisia za mapenzi ya dhati. Makala haya yamebaini kwamba, ukahaba ni miongoni mwa masuala yaliyosawiriwa kiuhalisia hakiki katika riwaya teule za Kezilahabi, mwandishi hajaishia tu kulisawiri jinsi lilivyo, bali analichambua, analikosoa na kubainisha madhara yake kwa washiriki hasa wanaume ambao aghalabu ndiyo huwatafuta makahaba hao. Mathalani, Tegemea ambaye ni kahaba anamaliza

pesa zote za Kabenga anazopewa na mwanawe. Isitoshe, bado anaomba hela nyingine za gauni. Kabenga anapojaribu kujitetea anafukuzwa kama mbwa. Anapoamua kutoa pesa za gauni, ndipo Tegemea anapojidai kumpenda na kumwita majina mazuri. Mwandishi anaibua hoja hii katika mazungumzo ya Kabenga na Tegemea kama inavyooneshwa katika dondoo lifuatalo:

> "Una tamaa sana ya pesa, yaani huwezi kumpenda mtu bila pesa. Huku shamba mwanamke hanunuliwi. Lakini mimi umenimalizia pesa zote anazoniletea mtoto wangu. Hata hivyo bado hutosheki. Sasa unadai gauni. Unafikiri mimi pesa nazitoa wapi?"
>
> "Kama jambo la gauni limekuudhi vaa suruali yako uende zako! Gauniii! Gauni! Gauni limekuwa gauni. Vaa suruali uende zako! Leo hufanyi jambo lolote nami. Yaani unafikiri mimi maskini omba-omba. Gauni!
>
> "Hasira yote hii ya nini?"
>
> "Nimesema v-a-a s-u-r-u-a-l-i u-ende zako!"
>
> Unataka kunitoa nje kana kwamba sikuzaa! Haya chukua!
>
> "He! He! He!" Tegemea alicheka. "Sasa hizi pesa umezitoa wapi? Bwana'ngu kila siku matata. Ngoja kidogo niweke mto wa pili."
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 70-71).

Mazungumzo baina ya Kabenga (baba yake Manase) na Tegemea katika dondoo hili yanaonesha dhahiri kwamba kahaba hana mapenzi ya dhati. Anashiriki zinaa ili apate pesa tu bila kujali mhusika anazitoa wapi na hali yake ikoje. Kezilahabi anawakosoa watu walio na fikra kama za Kabenga za kudhani kwamba kahaba anaweza kumhurumia mwanamume. Kwa hiyo, mwandishi anamchambua kahaba na kubaini kuwa hana huruma yoyote ile, yeye anajali pesa tu. Hili limejidhihirisha katika utetezi wa Kabenga anayejitetea kwamba pesa alizopewa na mtoto wake zote zimeisha kwa kumpa yeye; hata hivyo, Tegemea hajali hilo.

Mbali na makahaba kumaliza hela za wanaume, pia huwa na magonjwa. Hii ni kwa sababu kahaba hushiriki mapenzi na watu tofautitofauti kwa lengo la kupata pesa. Hivyo, ni rahisi kupata magonjwa. Hata hivyo, kwa kuwa kahaba anachoangalia ni pesa, hawezi hata kumwambia huyo anayetaka kushiriki naye tendo kwamba ni mgonjwa. Kwa mfano, Pili ambaye ni kahaba anawaambukiza ugonjwa Manase na Kazimoto. Mwandishi anadhihirisha hoja hii kupitia mazungumzo ya Manase na Kazimoto kama ifuatavyo:

> "Kazimoto, unamkumbuka yule msichana aitwaye Pili?"
>
> "Ndiyo," nilimjibu.
>
> "Basi siku moja nilitembea naye. Wakati huo alikwishapatwa na ugonjwa mbaya. Mimi bila kufahamu, usiku huohuo nilimwambukiza mke wangu. Kwa bahati mbaya mtoto aliumbika nyakati hizo za ugonjwa wangu. Wakati wa kuzaa ulipofika, tulimzaa mtoto huyu mwenye kichwa kikubwa ambaye ametushangaza." …
>
> Hapakuwa na haja ya kuficha mambo sasa. Nilimweleza jinsi nilivyokuwa nimezoea kutembea na Pili kabla na baada ya ndoa. Lakini nilimwambia kwamba mimi na mke wangu tulikuwa hatujasikia maumivu yoyote ya ugonjwa huo. Manase alinieleza kwamba ugonjwa huo ulikuwa hauwezi kutambulika kwa urahisi. Alisema kwamba ugonjwa huo unaingia ndani ya damu na kukaa bila kumdhuru mhusika" …
>
> **Chanzo:** *Kichwamaji* (1974: 191-192)

Dondoo hili linaonesha kwamba, Kezilahabi anakosoa tabia ya makahaba kujali pesa kuliko utu. Kwa mfano, Pili alijua kabisa yeye ana ugonjwa lakini hakuwaarifu Manase na Kazimoto kuhusu ugonjwa wake. Matokeo yake anasambaza ugonjwa huo kwa Manase na Kazimoto, ambao nao wanausambaza pia kwa wake zao. Kwa sababu ya ugonjwa huo, watoto wao wanazaliwa na vichwa vikubwa vya kushangaza. Ukosoaji huu wa Kezilahabi wa makahaba unaakisi Mkabala wa Uhalisia

Hakiki ambao unaeleza kwamba waandishi wa kiuhalisia hakiki hawaishii tu kusawiri hali ilivyo katika jamii, bali huichambua hali hiyo na hata kuikosoa.

Fauka ya hayo, makahaba huwadharau wale wanaoshiriki nao mapenzi hadi wake zao nyumbani. Kwa mfano, Hadija, kahaba aliyeshirikiana kimapenzi na Tumaini anamfuata nyumbani kwake na kuongea mambo yao bila hata kumwogopa mke wa Tumaini (Anastasia). Matokeo yake ni kuzua ugomvi baina ya Hadija na Anastasia. Mwandishi anatueleza suala hili katika dondoo lifuatalo:

> Jinsi Anastasia alivyotoka jikoni hakuna aliyefahamu, wala hapakuwa na mtu aliyemsikia akitembea. Walishtukia ukuni ukilia juu ya kichwa cha Hadija. "Malaya wewe! Toka! Hapa! Wewe ndiye unatuambukiza magonjwa!" Hadija alienea damu. Alijaribu kusimama ili apambane na Anastasia. Lakini Anastasia aliendelea kumpiga tena na tena kama mtu apigae nyoka. Hadija alianguka chini. John na Tumaini walipokumbuka kumshika Anastasia, Hadija alikuwa amekwisha haribika sura. "Acha nimwue! Mshenzi! Hii ni dharau kubwa sana! Malaya hawezi kuja kuzungumza mambo yake na bwana wangu mbele yangu! Waziwazi namna hii! Ala!"… Hadija aliamka. Aliinua gauni lake juu, na kati ya mwili wake na chupi alitoa bastola.
>
> Alifyatua! Pale pale Anastasia alianguka chini.
>
> "Mtoto wa mbwa! Unafikiri bwana wako ana nini! Anakupa nini ambacho mimi sipati! Hufahamu kwamba pesa za bwana wako huwa tunazigawana!" Hadija alikuwa akimwambia mtu ambaye alikuwa hasikii: Anastasia alikuwa amelala juu ya sakafu kama maiti.
>
> **Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975: 84)

Dondoo hili linaonesha dharau ya kushirikiana kimapenzi na kahaba. Kwa hiyo, Kezilahabi anakosoa wanaume ambao wameoa wanaoshiriki kimapenzi na makahaba namna wanavyoweza kuleta madhara kwao wenyewe na kwenye ndoa zao. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na dharau kwa mke wa ndoa, magonjwa na ugomvi baina ya mke na kahaba.

Ukosoaji huu wa suala la ukahaba unaakisi Mkabala wa Uhalisia Hakiki ambao unasema kwamba waandishi wa kihalisia hakiki hawaishii tu kusawiri hali ya kijamii, bali pia huchambua na kukosoa hali hiyo.

## Hitimisho

Makala haya yamefafanua masuala mbalimbali ambayo yamesawiriwa kiuhalisia hakiki katika riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) za Euphrase Kezilahabi. Katika kufafanua masuala hayo, mambo kadhaa yanajibainisha katika usawiri huo. Mosi, si masuala yote katika riwaya hizi ambayo yamesawiriwa kiuhalisia hakiki. Masuala ambayo yameonekana kusawiriwa kiuhalisia hakiki ni yale ambayo katika jamii yamegawanya mitazamo ya watu. Hivyo, anayasiwiri kiuhalisia hakiki ili kuchambua, kusaili na kukosoa mawazo tawala ambayo huyapuuza mawazo mengine. Pili, mtindo wa uhalisia hakiki uliojibainisha kutumika katika riwaya teule umemuwezesha mwandishi katika kutekeleza mambo matatu: kusaili, kukosoa na kuchambua. Tatu, mtindo wa uhalisia hakiki umemuwezesha mwandishi kuijuza hadhira yake upande pili wa mambo aliyoyaswiri. Mwisho, masuala yaliyosawiriwa kiuhalisia hakiki si yale yanayohusu maovu tu katika jamii. Mwandishi, kwa kutumia mtindo huu, amesawiri hata yale yanayochukuliwa kuwa ni mema au mazuri.

## Marejeleo


Arabi, S., Moghbel, A. G., Zareh, N., Balawi, R., na Pourabed, M. J. (2022). A Comparative Study of the Aspects of Critical Realism between *Yiki Boud Yaki Nabud* of Muhammad Ali Jamalzadeh and *Kan Ma Kan* by Mikhail Naima. *Biannual Journal.* Inapatikana katika https://doi.org/10.30465 /afg.2022.6771. Ilisomwa tarehe 10 Januari 2023.

Badru, Z. A. (2019). Uchunguzi wa Fumbo la Uhuru wa Mtu: Mifano kutoka Riwaya za Euphrase Kezilahabi. Katika A. S. Ponera na Z. A. Badru (Wah.), *Koja la Taaluma za Insia: Kwa Heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla* (481-507). Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.

Duwe, M. (2020). Usawiri wa Eskatolojia ya Waafrika katika Mbolezi za Wangoni. *Jarida la CHALUFAKITA, 2*, 158-173.

Gorky, M. (1949). *Mother*. Moscow: Progress Publishers.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Khalid, K. (1982). *The Prostitute in Progressive Literature*. London: Allison and Busby.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili; Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited na Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Mbiti, J. S. (1969). *African Religious and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Odongo, O. F. (2014). *Uchanganuzi wa Uwasilishaji wa Kifo katika Mashairi Teule ya Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno, Kisumu.

Quayson, A. (2000). *Postcolonialism: Theory, Practice or Process*. Cambridge: Polity Press.

Raphael, D. (2018). *Usawiri wa Ontolojia ya Kiafrika katika Ngano za Kiha*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Sanga, T. J. (2020). Dhima za Mbolezi za Sasa katika Jamii ya Wakinga Waishio Makete, Tanzania. *Kioo cha Lugha*, *18*, 208-228.

Sivananda, S. S. (1997). *What Become of the Soul After Death*. Himalayas: The Devine Life Society.

TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.